ISSN 1821-5866 ■ JANUARI - MACHI 2025

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
TANZANIA COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS AND GOOD GOVERNANCE

# THE VOICE OF Haki

JARIDA LA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA



# THBUB kushirikiana na wadau wengine

**NDANI** WATENDAJI 13756 WAFUNDWA KUHUSU HAKI ZA BINADAMU

# NENO LA UTANGULIZI

Nina furaha kuwakaribisha wasomaji wetu katika toleo la robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2024/2025 la Jarida la Sauti ya Haki linalotumika kufikisha habari na taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa majukukumu ya THBUB na masuala ya haki za binadmu na utawala bora.

Katika kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora, Tume ya Haki za binadamu na utawala bora imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha ulinzi na uhifadhi wa Haki hizo na utawala bora nchini. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa makundi mbalimbali katika Jamii. Makundi hayo ni pamoja na watendaji wa kata, wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo, waandishi wa habari na wananchi kwa ujumla.



**Mhe. Mathew Mwaimu (Jaji mstaafu)**
**Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Nitoe shukrani za dhati kwa Serikali ya awamu ya sita ikiongozwa na Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele katika kuiwezesha THBUB kutekeleza majukumu yake.

Aidha, nipende kutoa shukrani kwa wadau mbalimbali wa haki za binadamu na utawala bora nchini kwa ushirikiano wanaoutoa kwa THBUB. THBUB inawahimiza wadau wote kuendelea kushirikiana katika kulinda na kuhamasisha haki za binadamu na utawala bora ili kuendelea kuijenga jamii yenye kuheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

**Ninawatakia usomaji mwema.**

**KAMATI YA UHARIRI**
**Mwenyekiti:**
Monica Mnanka
**Mhariri:**
Zawadi A. Msalla
**Mhariri Msaidizi:**
Nuru Mfaume
**Wajumbe:**
Mwashamba Juma
Tumaini Obel
Farida Ruben

**MAWASILIANO**
Mtaa wa Nyerere,
Plot Na. 339/Kilimani
S.L.P 1049 DODOMA,
Tanzania
Simu: +255 738 279744
Barua Pepe:
www.chragg.go.tz

## YALIYOMO

WATENDAJI 13756 WAFUNDWA KUHUSU HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA — UK. 4
TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA, KUSHIRIKIANA NA WADAU WENGINE — UK. 5
KAMATI YA BUNGE YAJENGEWA UWEZO KUHUSU ELIMU YA HAKI ZA BINADAMU — UK. 6
THBUB YAONGEZA IDADI YA KLABU ZA HAKI ZA BINADAMU — UK. 7
THBUB YAFANYA UKAGUZI WA MAGEREZA NA VITUO VYA POLISI — UK. 8
THBUB YAHIMIZA USHIRIKIANO NA ASASI ZA KIRAIA ZINAZOTETEA HAKI ZA BINAADAMU — UK. 9
JAMII IZINGATIE USAWA WA KUMILIKI MALI BAINA YA WANAWAKE NA WANAUME — UK. 10

# Watendaji 13756 wafundwa

■ Na Mwandishi Wetu

Watendaji Kata 13756 kutoka katika Mikoa saba ya Tanzania wamepatiwa mafunzo ya Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora. Watendaji waliopatiwa mafunzo ni kutoka katika Mikoa ya Tabora, Kigoma, Singida, Iringa, Njombe, Dodoma na Manyara.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na THBUB yalilenga katika kuwakumbusha watendaji umuhimu wa kulinda haki za binadamu lakini pia kuzingatia misingi ya utawala bora katika utendaji kazi wao wa kila siku.

Katika, nyakati tofauti, Watendaji hao wameelezwa kuwa changamoto nyingi za uvunjwaji wa haki za binadamu zinachangiwa na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Watendaji katika nafasi zao za kiutendaji ni wakurugenzi wa kata, hivyo wana jukumu la kuhakikisha masuala ya uvunjwaji wa haki za binadamu katika maeneo yao yanakomeshwa.

Watendaji hao pia wamekumbushwa kuzingatia nguzo kuu za utawala bora kwa kuhakikisha wanakuwa na usawa, uwazi, watendaji wawajibikaji na utawala wa sheria. Katika mafunzo hayo watendaji walisisitizwa kuwa mstari wa mbele katika kuibua changamoto zinazojitokeza katika jamii .

Aidha, THBUB imewataka watendaji kutokuchukua maamuzi ambayo yanapaswa kuchukuliwa na ngazi za juu. Baadhi ya migogoro haipaswi kutatuliwa na watendaji pekee mfano migogoro ya ardhi.

Mafunzo hayo yaliyokuwa chachu kwa watumishi hao yameibua ari mpya ya utendaji kwa kuazimiwa na watendaji kuanza kufanya vikao vya mara kwa mara katika kata zao ili kupokea kero na hoja mbalimbali kutoka kwa wananchi na kuzipeleka katika ngazi zinazotakiwa katika zile ambazo hazitatatuliwa.

Katika mafunzo hayo, THBUB iliwapa nafasi watendaji kutoa maoni yao, na kuwasilisha kero wanazokutana nazo katika utendaji wao wa kazi kwa lengo la THBUB kushughulikia malalamiko hayo.



Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Nyanda Shuli akitoa elimu kuhusu misingi utawala bora kwa watendaji wa Kata zilizopo katika Halmashauri ya wilaya ya Kondoa na Halmashauri ya Kondoa Mji Mkoani Dodoma Machi 26, 2025.





Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Mhe. Mathew Mwaimu (Jaji Mstaafu) akizungumza na Rais wa Chama cha Wanasheria Adv. Boniface Mwabukusi pamoja na Wadau wa utetezi wa haki za binadamu Machi 17, 2025 Jijini Dodoma

# THBUB kushirikiana na wadau wengine kulinda, kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini

■ Na Mwandishi Wetu

Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Mhe. Mathew Mwaimu (Jaji Mst.) ameeleza kuwa THBUB itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kulinda na kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora kama vile sheria inavyowataka.

Amezungumza hayo alipokutana na Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) Wakili Boniface Mwabukusi na Ujumbe wa Wadau wa Utetezi wa Haki za Binadamu Machi 17, 2025 walipotembelea Makao Makuu ya Ofisi za THBUB Mtaa wa Kilimani jijini Dodoma

Mhe. Mwaimu amesema kuwa THBUB ni Taasisi ambayo hushirikiana na Wadau wa Taasisi za Kitaifa na Kikanda ili kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu katika Jamii na kusisitiza kuwa ushirikiano huo si wa hiari bali ni matakwa ya sheria ya Tume.

Pia, Mhe. Mwaimu ameongeza kuwa Serikali ndio mdau wa kwanza katika kulinda haki za binadamu ndio maana imeanzisha THBUB ili iweze kuisaidia katika kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kuheshimiwa nchini.

Awali, Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika, Wakili Boniface Anyisile Mwabukusi ameeleza lengo la ujio wao ni kuweka mikakati ya masharikiano na wadau wa utawala wa sheria, upatikanaji haki na utawala bora sambamba. Pia, ameanisha changamoto zilizopo katika eneo la upatikanaji wa haki, hususani kwenye haki jinai ili kutekeleza kwa pamoja kulingana na majukumu ya kila taasisi husika.

Kwa hatua nyingine Mhe.Mwaimu amepongeza ujumbe huo kwa kuja na wazo zuri la kushirikiana na wadau mbalimbali utakao saidia kuwahudumia wananchi kwa pamoja.



Kamati ya kudumu ya Bunge ya Utawala, Sheria na Katiba wakipatiwa elimu ya haki za binadamu na utawala bora, mafunzo hayo yaliyofanyika katika ukumbi mdogo wa Bunge la Jamhuri ya Munguano wa Tanzania mnamo Machi 24, 2025

# Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria yajengewa uwezo kuhusu elimu ya haki za binadamu na biashara

**Na Mwandishi Wetu**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imewajengea uwezo wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria juu ya Haki za Binadamu na masuala ya biashara nchini Machi 25, 2025. Lengo la mafunzo hayo yaliyofanyika katika Ukumbi mdogo wa Bunge Jijini Dodoma ni kuwawezesha wajumbe hao kupata uelewa wa namna ambavyo Tume imekusudia kulinda na kuboresha utekelezaji wa hali ya haki za binadamu nchini.

Akiwasilisha mada kwa niaba ya Tume, Bi. Jovina Muchunguzi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Utafiti na Nyaraka, ameeleza kuwa kumekuwa na changamoto zinazoathiri haki za binadamu ikiwa ni uchafuzi wa mazingira na ukiukwaji wa haki za wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kutopatiwa mikataba ya ajira na wajiri wao. Bi. Jovina alieleza namna ambavyo mpango huo umebainisha maeneo ambayo yatatakiwa kufanyiwa kazi na Serikali ili kuhakikisha hali ya haki za binadamu katika biashara inazingatiwa.

Mara baada ya wasilisho hilo, Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damasi Ndumbalo amepongeza Tume ya Haki za Binadamu kwa kufanya tafiti juu ya hali ya haki za binadamu na biashara nchini. Pia amesisitiza kuwa Serikali imefanya kazi kubwa katika nyanja za kujenga uchumi na mambo makubwa ambayo yanaonekana bayana na inaendelea kutekeleza.

"... upatikanaji wa Mpango kazi wa Kitaifa wa haki za binadamu na biashara umekuja kwa wakati muafaka wakati taifa likiwa linatekeleza miradi mikubwa ya kimkakati. Mlichokifanya leo mmeongelea kizazi cha pili cha haki za binadamu kinachohusika na haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Mada hii imewasilishwa ili kamati ipate uelewa juu ya Haki za binadamu na iweze kutambua kuwa tumefanya vizuri katika eneo la haki za binadamu..." amesema Dkt. Ndumbalo.

Kwa upande wao, wakizungumza kwa nyakati tofauti, wajumbe wa kamati wameipongeza THBUB kwa kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kuwataka kufanyia kazi changamoto zote zinazojitokeza katika kukwamisha wananchi kupata haki zao.



# THBUB yaongeza idadi ya klabu za haki za binadamu

**Na Mwandishi Wetu**

Katika kipindi cha miezi mitatu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imezindua jumla ya klabu 56 katika shule za msingi, sekondari na vyuo. Uzinduzi wa klabu hizo ni utekelezaji wa mikakati iliyojiwekea ya kukuza haki za binadamu nchini.

Klabu hizo zilizoanzishwa katika Mikoa ya Tabora, Manyara, Singida, Dodoma na Iringa hivi karibuni, zitakuwa ni chachu ya ulindaji na ukuzaji wa masuala ya haki za binadamu kwa watoto katika shule na vyuo husika.

Kamishna kutoka THBUB, Dkt. Thomas Masanja akieleza manufaa ya kujiunga katika Haki klabu, amesema pamoja na watoto kujifunza haki mbalimbali kama zinavyoainishwa katika Ibara ya 12- 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Dkt. Masanja anasisitiza kuwa kizazi kinachofahamu haki zake ndicho kizazi kinachoweza kupata maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa haraka.

"Serikali kupitia THBUB imedhamiria kujenga kizazi chenye uzalendo, kizazi kinacho fahamu utu wa mtu na kwamba hakuna maendeleo yanayoweza kupatikana pasipo na uzingatiaji wa haki na utawala bora" Alisema Dkt. Masanja.

> "Manufaa ya kujiunga katika Haki klabu, ni pamoja na watoto kujifunza haki mbalimbali kama zinavyoainishwa katika Ibara ya 12- 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Kamishna Dkt. Masanja amesisitiza kuwa THBUB ina amini kuwa wanafunzi waliojiunga katika klabu za haki za binadamu watakuwa mabalozi hata nje ya mazingira ya masomo yao.

" Hao wanaojiunga kama wanachama tunawategemea kuwa mabalozi wazuri hata wanapokuwa majumbani, kuhakikisha kuwa jamii zao zinaondokana na masuala ya uvunjifu wa haki za binadamu" Alisisitiza Dkt.Masanja

Dkt. Masanja amesisitiza pia kuwa wanachama hao watakuwa ni msaada mkubwa kuwasaidia watoto wanaoachishwa masomo kwa lazima na kupelekwa kufanya kazi za ndani au kuolewa. Pia, ameelezea changamoto iliyopokwa baadhi ya wazazi wanawanyima watoto wao haki ya kupata elimu na kuwaozesha wakiwa bado wadogo ili kujipatie fedha, jambo ambalo halikubaliki na ni kinyume na Sheria na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Utaratibu wa uanzishwaji wa klabu za haki za binadamu ulianza ukiwa na lengo la kutoa elimukwa wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo ambapo mpaka kufikia Machi 2025 jumla ya klabu 386 zimeanzishwa katika mikoa mbalimbali nchini.



Kamishna wa THBUB Mhe. Dkt Thomas Masanja akitoa elimu kuhusu haki za binadamu na utawala bora kwa walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mtwango iliyopo katika Halmashauri ya Njombe Vijijini, Mkoani Njombe, Machi 25, 2025.

# THBUB yafanya ukaguzi wa magereza na vituo vya polisi

**Na Mwandishi Wetu**

THBUB imefanya ukaguzi wa magereza 12 ikiwa ni utekelezaji wa moja ya majukumu ambayo yameanishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu inayoitaka Tume kufanya kaguzi mahali wanapozuiliwa watu.

Kazi ya ukaguzi wa magereza na vituo vya polisi inayofanywa na THBUB, imekuwa na mafanikio makubwa hasa katika uboreshaji wa utoaji haki na mazingira wanayoishi wafungwa na watumishi wa magereza na polisi.

Akizungumzia kuhusu jukumu hili la ukaguzi wa magereza na vituo vya polisi, Makamu Mwenyekiti wa THBUB, Mhe. Mohamed Khamis Hamad alisema kila ukaguzi unapofanyika, THBUB huandaa ripoti na kuipeleka katika mamlaka zinazohusika ili kuhakikisha changamoto zinazobainika katika maeneo hayo zinatatuliwa.

Masuala yanayoangaliwa katika kaguzi za magereza na vituo vya polisi ni pamoja na kukagua mabweni ya wafungwa na mahabusu kama yana kidhi ubora wa kulala wanadamu, mavazi, chakulana kusikiliza kero na kupokea malalamiko kutoka kwa mahabusu, wafungwa na watumishi.

”Hatuishii kwa wafungwa na mahabusu tu, bali huwa tunakagua makazi ya askari na pia kuongea nao ili waweze kuwasilisha mambo yale ambayo yamekuwa ni kikwazo kwao katika utendaji kazi” Alisema Mhe. Makamu Mwenyekiti.

Aidha, Mhe. Mohamed alisema yapo mafanikio yaliyopatikana kutokana na kaguzi zinazofanyika.

” Unapoona wafungwa wanavaa mavazi haya waliyo nayo sahizi tambua ni jitihada za THBUB katika kulinda utu wa mtu, hapo awali wafungwa walikuwa wakivaa kaptula . THBUB imetoa mchango mkubwa sana katika kubadilisha mavazi na kuboresha malazi ya wafungwa na mahabusu” Alisema Mhe. Mohamed.

Mhe. Mohamed alieleza kuwa THBUB ipo katika mchakato wa kufanya kikao kikubwa na viongozi wa juu Serikalini pamoja na magereza na Polisi ili kuangalia namna ya kutatua changamoto zilizobainika.



UJUMBE wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ukiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Kituo cha Polisi Manyoni mkoani Singida ulipofanya ziara wilayani humo Januari 31, 2025. Kulia ni Afisa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Nasembo Kazeni na Mwakilishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Alnachius Bagenda (kushoto).



# THBUB yahimiza ushirikiano na asasi za kiraia zinazotetea haki za binaadamu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Ofisi ya Zanzibar, Mhe. Khatib M. Mwinyichande amesifu ushirikiano uliopo baina ya THBUB na jumuiya zisizo za Serikali zinazotetea haki za binaadamu.

Amesema, ushirikiano wao utaongeza nguvu ya pamoja katika kueneza elimu kwa umma ili kuifika jamii iliyokusudiwa kwa wakati.

Aidha, ameeleza kuwepo kwa nguvu ya pamoja juu ya mapambano ya utetezi wa haki za binaadamu zinahitajika ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na taasisi hizo.

Mhe. Mwinyichande aliyasema hayo wakati kikao wa pamoja wa ushirikiano baina ya taasisi za haki jinai na watetezi wa haki za binaadamu wakiwemo wenyeji Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora, (THBUB), Jumuiya ya Mawakili Zanzibar - (ZLS), Jumuiya Wanasheria wa Afrika, Jumuiya ya Mawakili kutoka Afika Mashariki, (EALS) na Chama cha Wanasheria Wanawake, Zanzibar (ZAFELA) kilichofanyika ofisi ya (THBUB) Mbweni Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi Machi 24, 2025.

Aidha, aliongeza kuwa ukaribu uliopo baina ya THUBU na taasisi hizo katika kubadilishana uzoefu na kuunganisha nguvu katika utetezi, upatikanaji wa haki za binaadamu na kutoa elimu kwa wadau wengine wa haki za binaadamu utakuwa chachu katika kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Naibu Katibu Mtendaji THBUB, Juma Msafiri Karibona amezishukuru taasisi hizo kwa ujio wao kwenye Ofisi za THBUB sambamba na kusisitiza ushirikiano wao hasa kwenye utetezi wa haki za binaadamu.

Naye, Mratibu Taifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, Wakili Onesmo Olengurumwa amepongeza jitihada za pamoja katika kulinda na kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora . Pia, ametoa rai ya kuongeza nguvu ya pamoja kwenye uchunguzi na hatua za haraka endapo kutabainika uvunjifu wa haki za binaadamu.

Kwa upande wake, Afisa Mfawidhi na Afisa Mchunguzi Mkuu (THBUB) Zanzibar, Saada Ahmeid Masoud amehimiza ushirikiano zaidi baina ya taasisi hzi kwenye utetezi wa haki za binaadamu na utawala bora.

Taasisi nyengine zilizoshiriki kwenye kikao cha pamoja cwa ushirikiano katika utetezi wa haki za binaadamu ni East Afican Law Society (EALS), Pan African Lawyers Union (PALU), Chama cha Wanasheria Wanawake (ZAFELA) na Tanganyika Law Society (TLS).

# Waandishi Manyara wakumbushwa wajibu wao kulinda haki za binadamu

**Na Mwandishi Wetu**

Makamu Mwenyekiti wa Tume za Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mhe. Mohamed Khamis Hamad ametoa rai kwa waandishi wa Habari wa Mkoa wa Manyara kutumia elimu ya haki za binadamu walioipata kuielimisha jamii na kutoa taarifa ya vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Rai hiyo imetolewa wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wandishi hao kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora yaliyotolewa katika ukumbi wa mikutano wa Mkuu wa Mkoa wa Manyara Machi 19,2025.

“Elimu kuhusu haki za binadamu ni nyenzo muhimu ya kuhakikisha kuwa wananchi wanazitambua na kulinda haki zao............” amesema Mohamed.

Naye Mchunguzi Mkuu Msaidizi wa Tume ya Haki za binadamu, Bw. Halfan Botea, wakati wa uwasilishaji wa mada ya haki za Binadamu amefafanua kuwa ukiukwaji wa haki moja huathiri haki nyingine.

Hivyo, amesisitiza kuwa jamii inapaswa kuzingatia haki za binadamu ili kuwa na jamii yenye amani na utulivu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya waandishi wa habari walioshiriki mafunzo hayo wameiomba Tume kuendela kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu masuala ya haki za binadamu kwa waandishi wa habari nchini kwa kuwa kundi hili ni wadau muhimu katika kulinda na kutetea haki za binadamu katika jamii.

Mafunzo yaliyotolewa kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Manyara ni mwendelezo wa utoaji wa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa kundi hilo katika mikoa ya Tabora, Singida, Iringa, Njombe, Kigoma na Dodoma.

# Jamii izingatie usawa wa kumiliki mali baina ya wanawake na wanaume

■ **Na Mwandishi Wetu**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeitaka Jamii kutambua usawa wa wanawake na wanaume katika kumiliki mali.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Malalamiko na Uchunguzi Bi. Suzana Ndeona (THBUB) wakati akitoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora wakati wa maonesho ya taasisi za Serikali na binafsi kuelekea maadhimisho ya Siku wanawake Duniani yaliyofanyika kitaifa Machi 08, 2025 Mkoani Arusha .

Bi. Ndeona ameielezea jamii kuwa sheria za Tanzania zinaruhusu na kutambua haki ya mwanamke kumiliki na kurithi mali lakini bado kumekuwa na changamoto ya utekelezaji wake kutokana na kuwepo kwa mila na desturi potofu na kandamizi kwa wanawake.

Akibainisha changamoto zinazwakabili wanawake Bi. Ndeona amesema kuwa bado wanawake wengi wana uelewa mdogo kuhusu haki zao kisheria licha ya elimu kubwa inayotolewa kwao.

"...ni muhimu sisi wanawake tukatambua kwamba tuna haki sawa na wanaume hususan kwenye kumiliki mali ikiwemo mashamba, nyumba na hata kurithi mali kama wanavyofanya wanaume, kujua haki yako inasaidia kufikia usawa wa kijinsia na maendeleo endelevu." Amesema Bi Ndeona

Aidha, Bi. Ndeona amewasihi wanawake kujithamini kwa kutambua kuwa mali hazina jinsia, hivyo wanapaswa kutumia fursa zilizopo kujiendeleza na kujikomboa kiuchumi.



Watumishi wanawake THBUB Tawi la Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Kitaifa yaliyofanyika katika viwanja vya Leaders Club, Jijini Dar es salaam Machi 8, 2025.



Watumishi wanawake THBUB Makao Makuu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Kitaifa yaliyofanyika katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Mkoani Arusha Machi 8, 2025.





Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Bw. Balandya Mayuganya akisaini kitabu cha wageni mara wakati alipotembelea banda la THBUB baada ya uzinduzi wa Maonesho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea katika Viwanja vya Nyamagana Mjini Mwanza Januari 25, 2025



MKURUGENZI Msaidizi wa Idara ya Elimu kwa Umma na Mawasiliano wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Zawadi Msalla akizungumza na wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Kaliua mkoani Tabora wakati wa ziara ya THBUB hiyo wilayani humo hivi karibuni.



Afisa Uchunguzi Mkuu Bw. Ramadhan Slaa akitoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Daya vilivyopo Vitongoji, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba Machi, 2025.



Afisa Elimu Kazi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu Bi. Tulia Msemwa akiongoza wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi THBUB kuchagua Wajumbe Wapya wa Baraza la wafanyakazi la THBUB Januari 28, 2025 baada ya wajumbe waliokuwepo kumaliza muda wao.



Kamishna wa Tume za Haki za Binadamu, Mhe. Nyanda Shuli (kushoto), Katibu Msaidizi THBUB, Bw. Juma Karibona) wa pili kulia na Mkurugenzi wa Idara ya Elimu kwa Umma, Mawasiliano, Tafiti na Nyaraka, Bi. Monica Mnanka wakifuatilia mafunzo ya kulinda na kuhifadhi haki za binadamu yalifanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma India Machi 03 hadi 08, 2025.





Wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Uandaaji wa Mpango kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu na Biashara wakipokea taarifa ya mpango huo kutoka kwa Timu ya Wataalam ya uandaaji wa Mpango kazi wa Kitaifa wa haki za binadamu na biashara, Jijini Dar es Salaam, Februari 21, 2025.

# Kamati ya kitaifa ya usimamizi wa uandaaji mpango kazi wa kitaifa wa haki za binadamu na biashara yaidhinisha rasimu ya mpango

**Na Mwandishi Wetu**

Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Uandaaji wa Mpango kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu na Biashara ikiongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dkt. Franklin J. Rwezimula ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria imeidhinisha rasimu ya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu na Biashara.

Rasimu hiyo imekabidiwa na Timu ya Wataalam ya kuandaa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu na Biashara katika kikao kazi kilichofanyika Jijini Dar es Salaam Februari 21, 2025.

Akizungumza na waandishi wa habari, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Mohamed Khamis Hamad ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati hiyo amesema, mpango kazi huo unaangazia shughuli zote muhimu za kiuchumi zinazoweza kumuathiri mwanadamu.

“Tanzania inakuwa kiuchumi, hivyo ni muhimu kuangazia ni vipi hizi shughuli za kiuchumi zitakwenda sambamba na haki za watu, kam vile tunavyosikia kwamba kuna migogoro ya wawekezaji na wananchi wa maeneo ya karibu, kuna wengine hawapewi mikataba ya kazi, wengine hawana vifaa vya kujilinda wakati wa kazi, kuna maswala ya kimazingira, hizo zote ni shughuli za kibiashara ambazo kwa njia moja au nyingine zinaweza kumuathiri huyu mwanadamu “. Amesema Mhe. Hamad

Naye, Dkt. Noel Komba, Mchumi Mkuu kutoka Wizara ya Fedha ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati amesema rasimu hiyo ipo katika hatua za mwisho na matarajio ni kwamba baada ya kukamilika, mpango huo utatoa fursa kwa Wawekezaji katika sekta mbalimbali na wananchi ambao ni waajiriwa pale wanapopata migogoro ya haki zao katika maeneo yao ya kazi.

Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa uandaaji wa mpango kazi wa kitaifa wa haki za binadamu na biashara ina wawakilishi kutoka Tanzania bara na Zanzibar ambapo ndani yake kuna wajumbe kutoka Serikalini, Taasisi za Serikali, sekta binafsi, mashirika ya kiraia na wataalam wa masuala ya haki za binadamu na biashara.



Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Amina Talib Ali atoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Kanyonza wilaya ya Kakonko Mkoani Kigoma Februari 21, 2025.

# Wazazi waaswa kulinda maadili ya watoto

**Na Mwandishi Wetu**

Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Amina Talib Ali ametoa wito kwa wazazi na walezi kutimiza jukumu lao la kulea na kulinda maadili ya watoto wao ili kukomesha vitendo vya uvunjifu wa maadili katika Jamii.

Kamishna Amina ametoa wito huo wakati akitoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora katika Mkutano wa Hadhara uliofanyika Kata ya Kanyonza iliyopo wilayani Kakonko Mkoani Kigoma Februari 21, 2025.

"...ni jukumu letu wazazi kuhakikisha kuwa tunafahamu watoto wetu wanapokwenda, muda anaotoka na

> “ Tunatakiwa kufanya kazi ya kutafuta pesa lakini pia tukumbuke kutenga muda wa kukaa na Watoto

kurudi nyumbani na tuna wajibu wa kukaa na kuzungumza na o juu ya changamoto na vishawishi wanavyovipata wakiwa shule na hata maeneo yawayocheza ....". Amesema Mhe.

Wito umetolewa pia kwa wazazi kushirikiana na taasisi zote ziazohusika na watoto katika jukumu la kujenga maadili kwa watoto.

"Tunatakiwa kufanya kazi ya kutafuta pesa lakini pia tukumbuke kutenga muda wa kukaa na Watoto, Watoto wengi wanakatisha masomo kwa sababu ya kunyanyaswa kingono wengine kupatiwa mimba wakiwa bado wanasoma. Haya yote yanatokea kwa sababu wazazi na walezi tumesahau wajibu wetu kama walinzi na wasimamizi wa maadili ya watoto wetu" amesema Mhe. Amina



# Maswi aitaka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuwa taasisi ya mfano

**Na Mwandishi Wetu**

Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Eliakim Maswi amewataka watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) kufanya kazi kwa kuzingatia sheria za nchi, maadili na nidhamu ya kazi.

Maswi ametoa wito huo wakati akifungua Mkutano wa 23 wa Baraza la Wafanyakazi wa uliofanyika katika Ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Februari 5, 2025.

" kazi mliyonayo ni kuithibitishia Serikali kwamba mko tayari kutekeleza majukumu mliyopewa kwa mujibu wa sheria na mnatakiwa kuwa mfano bora wa kuigwa kwa kuwa taasisi inayolinda haki za binadamu na misingi ya utawala bora " amesisitiza Maswi

Awali akitoa neno la utangulizi, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Bw. Patience Ntwina amesema kuwa lengo la mkutano huo ni kupitia na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za Tume kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 na na mapendekezo ya mpango na bajeti ya mwaka 2025/2026.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa baraza la wafanyakazi (TUGHE) tawi la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Bw. Pontian Kitorobombo, kwa niaba ya Wajumbe wa baraza hilo amemshukuru Katibu Mkuu kwa kufungua Mkutano huo na kuahidi kuwa wajumbe watahakikisha wanaisaidia taasisi kuwa kwa kujadili masuala yenye kuleta tija kwa taasisi na watumishi.



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi ambaye pia ni Katibu Mtendaji THBUB Bw. Patience Ntwina akitoa neno la utangulizi kabla ya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la 23 la Wafanyakazi wa THBUB uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Februari 05, 2025. Kulia kwake ni Katibu Msaidizi THBUB, Bw. Juma Msafiri Karibona.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bw. Eliakim Maswi (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la 23 la Wafanyakazi THBUB mara baada ya ufunguzi wa Baraza hilo Jijini Dodoma, Februari 05, 2025.

**MAWASILIANO**
Mtaa wa Nyerere, Plot Na. 339/Kilimani
S.L.P 1049 DODOMA, Tanzania
Simu: +255 738 279744
Barua Pepe:
www.chragg.go.tz